#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 7

Julai - Septemba 2022



# SAMIA SCHOLARSHIP HABARI YA MJINI

**Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam**

Ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan juu ya mageuzi ya sekta ya elimu yameanza kujidhihirisha kufuatia Serikali kutenga kiasi cha TZS 3 bilioni ikiwa ni ruzuku ya kusomesha wanafunzi 640 kupitia ufadhili wa 'Samia Scholarship'.

Ufadhili huo mpya unaosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia unalenga fani za sayansi kupitia kwa wanafunzi wenye ufaulu mkubwa katika mitihani ya kuhitimu kidato cha sita katika masomo ya sayansi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza katika uzinduzi wa maombi ya Programu hiyo hivi karibuni Jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema ufadhili huo ni mpya kwa masomo ya shahada ya kwanza nchini na kuongeza kati ya wanafunzi hao; wavulana ni 396 na wasichana ni 244.

**Serikali kutenga kiasi cha TZS 3 bilioni ikiwa ni ruzuku ya kusomesha wanafunzi 640 kupitia ufadhili wa 'Samia Scholarship'**

**Prof. Adolf Mkenda alisema ufadhili huo ni mpya kwa masomo ya shahada ya kwanza nchini na kuongeza kati ya wanafunzi hao; wavulana ni 396 na wasichana ni 244.**

**...katika hotuba yake aliyoitoa Bungeni Aprili 22, 2021, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliainisha dira, dhamira, mwelekeo na vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita**

"Wanafunzi hawa watalipiwa asilimia 100 ya gharama zote za masomo katika kipindi chote cha masomo yao ikiwemo ada ya Mafunzo, posho ya chakula na malazi, posho ya Vitabu na Viandikwa, Mahitaji Maalum ya Vitivo, Mafunzo kwa Vitendo, Utafiti, Vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na Bima ya Afya" alisema Prof. Mkenda.

Kwa mujibu wa Profesa Mkenda amesema miongoni mwa sifa kuu za kupata ufadhili wa Samia Scholarship ni pamoja na mwanafunzi kupata udahili katika programu za masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Tiba katika Chuo Kikuu hapa nchini kinachotambuliwa na Serikali.

Itakumbukwa kuwa katika hotuba yake aliyoitoa Bungeni **Aprili 22, 2021**, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliainisha dira, dhamira, mwelekeo na vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi huku sekta ya elimu ikipewa msukumo mkubwa zaidi.

Ni Dhahiri kuwa kuanzishwa kwa mpango wa 'Samia Scholarship' ni utekelezaji wa dhamira ya Mhe. Rais kuhakikisha kuwa sekta ya elimu inakidhi mahitaji halisi ya Watanzania sambamba na kuongeza msukumo wa kuhakikisha kuwa watu wote wanapata elimu.

Katika mwaka wa masomo 2022/2023 Serikali kupitia HESLB imetenga TZS 570 bilioni kwa ajili utoaji wa mikopo kwa wanafunzi watakojiunga na masomo ya elimu ya juu katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu nchini.

## JAMBO LETU



– **Ismail Ngayonga**
*Mhariri*

# "POCHI LA MAMA" LIMEFUNGUKA

Sio siri kuwa vijana ni kundi muhimu katika taifa lolote duniani. Hii ni kwa sababu, kitakwimu, vijana wapo wengi na kwa takwimu za sasa, nchi yetu inakadiriwa kuwa na vijana wapatao milioni 21.

Ukiachilia mbali takwimu hizo, vijana ni nguvu kazi ya taifa; ni walinzi wa taifa; ni watu wenye ubunifu, wana uthubutu, ni wajasiri na ndiyo waliobeba maono na matarajio ya Taifa kwa sasa na siku zijazo.

Kwa maneno mengine, uhai, usalama, maendeleo na ustawi wa taifa lolote duniani unawategemea vijana. Hakuna taifa linaloweza kusonga mbele bila kutegemea vijana wake.

Pamoja na ukweli huo, kundi hili la vijana linakabiliwa na changamoto nyingi na mojawapo ya changamoto hiyo ni elimu na ukosefu wa ujuzi, ambapo katika kushughulikia suala hili la elimu na ujuzi, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kila mwaka.

Hivi karibuni, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizindua programu ya ufadhili wa masomo ya elimu ya juu ijulikanayo kama 'Samia Scholarship' ambapo kiasi cha TZS 3 Bilioni kimetengwa na Serikali kwa ajili ya ruzuku ya ufadhili kwa wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi masomo ya sayansi katika mitihani ya kuhitimu kidato cha sita kwa mwaka 2022/2023.

Kupitia ufadhili huo Serikali italipa gharama zote za masomo ikijumisha ada ya mafunzo, posho ya chakula na malazi, posho ya Vitabu na Viandikwa, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo, utafiti, vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na Bima ya Afya.

Ni wazi kuwa "pochi la Mama linazidi kufunguka" kwa vijana, hivyo ni wajibu wa wanafunzi wahitaji kuweka bidii ya masomo na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuzalisha wataalamu wa kada muhimu katika maendeleo ya taifa letu.

Menejimenti ya HESLB itaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kkuwahudumia wanafunzi katika msimu wa maombi ya mikopo kwa mwaka 2022/2023.

## NDANI...



03 KISWAHILI CHAPAISHWA



05 ALICIA: TUTASIMAMA NA RAIS SAMIA




06 PROF. MKENDA AZINDUA MRADI WA HEET

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Ismail Ngayonga
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Jacqueline Msuya

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Mkurugenzi Mtendaji
Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, TAZARA
S.L.P 76068
Dar es salaam
Tanzania

**Simu:** 0739 665 533
**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz
**Tovuti:** heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



Ukusanyaji wa mikopo iliyoiva nao umeongezeka kutoka wastani wa TZS 2 bilioni kwa mwezi mwaka 2015/2016 hadi TZS 17 bilioni kwa mwezi mwaka 2021/2022.

# TUTAENDELEZA UFANISI, UBORA NA UMAKINI WA HUDUMA KWA WATEJA

Mpendwa msomaji wetu karibu tena katika toleo Na. 7 la Jarida la mtandaoni la HESLB Yako ambalo kimsingi ni daraja la mawasiliano baina ya HESLB na wadau wetu.

Tarehe 12 Julai mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alizindua dirisha la maombi ya mkopo msimu sambamba na mwongozo wa maombi ya mikopo kwa msimu wa mwaka 2022/2023.

Tunapoanza msimu mpya wa masomo 2022/2023, dhamira ya Menejimenti ya HESLB ni kuongeza ufanisi katika kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma zetu ili kukidhi haja na matarajio ya wateja wetu.

Dhamira yetu ni kukushirikisha na kupokea maoni yako ili kuboresha huduma zetu. Ni kwa kuzingatia hili, tumekuwa tukitekeleza Mpango Mkakati wetu wa miaka mitano (2022/2023 – 2026/2027) ambao unaongozwa na nguzo kuu tatu: Mosi, Kuboresha mifumo ya uendeshaji (Business Processes Re-engineering); Pili, Kukusanya na kutoa mikopo zaidi (Optimal Lending & Collection); na tatu Kuimarisha mahusiano ya kimkakati (Strategic Partnerships).

Ili kutimiza nguzo hizo, wewe msomaji ni mdau muhimu sana kwetu. Ninakusihi utumie muda wako kusoma na kutupatia maoni kupitia mawasiliano yaliyopo katika jarida hili. Tunakuahidi tutayafanyia kazi.

Uboreshaji mkubwa wa mifumo umeendelea kwa awamu mbili, (Grand Automation & Systems Intergration Phase I & II). Kwa sasa maombi yote ya mikopo yanafanyika kwa mtandao na mwombaji anapata taarifa kupitia akaunti yake mtandaoni.

Katika kipindi cha miezi michache iliyopita, mteja ameweza kujua deni lake na kurejesha kupitia simu ya mkononi. Pili, kuhusu kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi, kwa mwaka 2021/2022, wanufaika walikuwa 177,889 wakati mwaka 2014/2015 walikuwa 98,300.

Ukusanyaji wa mikopo iliyoiva nao umeongezeka kutoka wastani wa TZS 2 bilioni kwa mwezi mwaka 2015/2016 hadi TZS 17 bilioni kwa mwezi mwaka 2021/2022. Aidha mahusiano na wadau wetu yameimarishwa. Wadau hao ni wanafunzi, serikali za wanafunzi na mashirikisho yao – TAHLISO na ZAHLIFE.

Wadau wengine ni vyuo, waajiri, taasisi za fedha na mashirika na taasisi mbalimbali. Wewe ni mdau muhimu. Tunahitaji maoni yako.

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha 10 duniani zenye idadi kubwa ya wazungumzaji duniani. Inakadiriwa kuwa hadi sasa Kiswahili kina zaidi ya wazungumzaji Milioni 200.




# KISWAHILI CHAPAISHWA

Serikali imesema katika mwaka wa masomo 2022/2023 wanafunzi watakaosoma masomo ya lugha Kiswahili katika vyuo vikuu nchini watapewa kipaumbele katika upangaji na utoaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mwongozo wa uombaji mikopo kwa mwaka 2022/2023, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema hatua hiyo inatokana na ukuaji wa lugha ya Kiswahili duniani na mahitaji ya wataalamu katika kukidhi mahitaji ya soko kitaifa na kimataifa.


"Baada ya dunia kuadhimisha siku ya Kiswahili tarehe 7 Julai mwaka huu, imepanga katika mwaka wa masomo 2022/2023 wanafunzi wote wanakaosoma Kiswahili na ukarimu watapewa kipaumbele katika kundi la kwanza katika utoaji mikopo" amesema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda amesema malengo ya Serikali ni kuzalisha wataalamu wengi wenye uwezo wa kuongea na kutafsiri lugha mbalimbali ili kuiwezesha lugha hiyo kuongeza idadi ya wazungumzaji duniani.

Akifafanua zaidi Prof. Mkenda amesema kutokana na msisitizo uliowekwa na Serikali katika kuipaisha lugha hiyo, kwa mwaka wa masomo 2022/2023 wanafunzi wote wanakaosoma masomo ya lugha ya Kiswahili watakuwa katika kundi moja la ushindani katika upangaji mikopo pamoja na wanafunzi waliosoma masomo ya kemia, fizikia na hisabati.

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha 10 duniani zenye idadi kubwa ya wazungumzaji duniani. Inakadiriwa kuwa hadi sasa Kiswahili kina zaidi ya wazungumzaji Milioni 200.

Tarehe 23 Novemba, 2021 Shirika la Umoja wa Mataifa la elimu, sayansi na utamaduni (UNESCO) lilitangaza rasmi tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku ya Kiswahili duniani.




*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa tatu kulia) akizindua nembo ya Mradi wa miaka miaka wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) katika hafla iliyofanyika tarehe 13 Septemba, 2022 Jijini Dar es Salaam.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael akisalimiana na baadhi ya Watendaji waandamizi wa HESLB wakati wa ziara yake aliyoifanya katika Ofisi za HESLB tarehe 21 Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam.*




*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda akizindua mwongozo wa utoaji na upangaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka 2022/2023 wakati wa hafla iliyofanyika katika Ofisi za HESLB Tazara Jijini Dar es Salaam tarehe 12 Julai, 2022.*



*Afisa Usafirishaji Mwandamizi wa HESLB, Juma Mohamed akitoa ufafanuzi kwa wateja waliotembelea Banda la HESLB wakati wa maonesho ya wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika Viwanja vya Mapinduzi Square tarehe 18-24 Juni, 2022.*



*Afisa Mikopo wa HESLB, Deonista Komba akitoa ufafanuzi kwa wateja waliotembelea Banda la HESLB wakati wa maonesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika tarehe 18-23, Julai, 2022 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam. Maonesho hayo yaliandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).*



# ALICIA:
## TUTASIMAMA NA RAIS SAMIA

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Serikali ya Jumuiya ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu John (SOSJUT) umeishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga na kuongeza kiwango cha fedha za bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB Yako, Rais wa (SOSJUT) Alicia Mwami amesema hatua ya Serikali kupitia HESLB kutoa fedha za mikopo kwa wanafunzi inatokana na dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu.

"Tunamshukuru Mhe Rais Samia kutokana na Serikali kuendelea kutenga na kuongeza fedha za bajeti ya mikopo mwaka hadi mwaka, SOSJUT tunampongeza Mhe. Rais na tunaahidi kutimiza wajibu wetu kwa kusoma kwa bidii kwani fedha hizi ni kodi za wananchi" amesema Alicia.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa mikopo chuoni hapo, Alicia amesema fedha za mikopo kutoka HESLB zimekuwa zikilipwa kwa wakati na uongozi wa jumuiya hiyo umekuwa ukipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa menejimenti ya Chuo pale panapojitokeza changamoto zinazohusu mikopo kwa wanafunzi.

Aidha Alicia amesema Jumuiya hiyo imekuwa ikifanya matamasha mbalimbali yenye malengo ya kuwakumbusha wanafunzi kutambua wajibu wao kwa kuhakikisha wanatumia fedha zinazotolewa na HESLB katika malengo yaliyokusudiwa.

Katika hatua nyingine Alicia ameiomba HESLB kuweka utaratibu wa kukutana mara kwa mara na viongozi wa Serikali za Wanafunzi pale panapokuwepo na mabadiliko ya matumizi ya mifumo ya taarifa katika utoaji na upangaji mikopo kwa wanafunzi.

Chuo Kikuu cha Mtakatifu John (SJUT) kina jumla ya wanafunzi 2,566 wanasoma masomo ya shahada za kwanza chuoni hapo.

"Tunamshukuru Mhe Rais Samia kutokana na Serikali kuendelea kutenga na kuongeza fedha za bajeti ya mikopo mwaka hadi mwaka, SOSJUT tunampongeza Mhe. Rais na tunaahidi kutimiza wajibu wetu kwa kusoma kwa bidii kwani fedha hizi ni kodi za wananchi" amesema Alicia.




# PROF. MKENDA
## AZINDUA MRADI WA HEET

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali itahakikisha inawasomesha Wahadhiri wa Vyuo Vikuu nje ya nchi Ili kusaidia kutoa elimu na ujuzi yenye kiwango bora kuendana na soko la ajira kimataifa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Mradi wa HEET Prof Mkenda amesema mradi huo unalenga katika kuleta mageuzi katika sekta ya elimu ya juu nchini na utatekelezwa katika taasisi za elimu ya juu (22.

Amesema Ili kusaidia kuongeza ubora wa Elimu na lazima ianzie juu ndipo ishuke sekondari hadi shule za msingi kwani dunia sasa hivi imebadilika kinachohitajika ni ujuzi zaidi.

"Duniani kote wanazungumzia suala la elimu, hii inatokana na changamoto ya kuwa na wahitimu wengi lakini wanaoshindwa kujiajiri kutokana na kutokuwa na ujuzi. Ukitazama vyeti wanavyo lakini mwanafunzi inashindikana kujiajiri. Hivyo Wahadhiri waliopata fursa kwenda kusoma nje wakihitimu wanaokuja kubadilisha mtazamo" alisema Waziri Mkenda.

Sanjari na hayo Waziri Mkenda amesema Mradi huo ni mkubwa na ni wa kipekee ambao umekuja kutoa hamasa na kusukuma Tanzania katika suala zima la elimu ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vyuo na mitaala.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael amewataka wasimamizi wa mradi kuhakikisha fedha zikizotolewa za mradi zinatumika katika lengo lililokusudiwa kwani ikibainika kuna ujanja ujanja watakaohusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Amebainisha kuwa jumla ya Dola 425 sawa na Bilioni 972 zimetolewa na Benki ya dunia ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kwa lengo la kuboresha elimu ya juu.

Naye Mwakilishi kutoka benki ya Dunia, Preeti Arora ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuwa na mtazamo chanya wa kuboresha elimu ili kuendana na mahitaji ya Soko la ajira la kimataifa na kwamba watahakikisha wanashirikiana nao bega kwa bega pale watakapohitajika.

# PATSON SANGA

## NAUTAMANI UHANDISI UMEME



**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

WANAZUONI wana msemo maarufu unaosema "Tafuteni Elimu hata kama ni China", ikitafsiriwa kuwa tafuta elimu bila kujali umbali wa safari ya kuipata.

'Engineer' Patson Sanga (22) anasafiri kutoka Kijiji cha Igolwa Wilaya ya Makete Mkoani Njombe hadi Mkoani Mbeya kuianza safari iliyojawa na matumaini ya kuifikia ndoto yake kusoma fani ya uhandisi wa umeme huku akitoa shukrani zake kwa serikali kupitia HESLB kwa kumpatia mkopo wa elimu ya juu.

"Naishukuru HESLB kunipatia mkopo wa elimu ya juu kwani hii imechochea shauku ya ndoto niliyonayo ya kuwa Mhandisi wa masuala ya umeme hapo baadae hadi" amesema Patson Paulo Sanga, mtoto wa kwanza ya familia ya Mzee Paulo Sanga (45).

Patson amesema HESLB imebeba tumaini la ukombozi wa kielimu kwa wanafunzi wa familia za hali ya chini kiuchumi kwani wengi wao wanategemea mikopo katika kumudu gharama za masomo ikiwemo ada ya masomo na gharama nyinginezo. "Binafsi nakiri kuwa bila mkopo wa HESLB nisingeweza kusoma masomo ya Chuo Kikuu" amesema Patson.

Amesema ni vijana wachache sana wa Kijijini kwao waliofanikiwa kufika ngazi ya Chuo Kikuu kwani wengi wao waliishia elimu ya msingi kutokana na changamoto ya mazingira ya hali ya hewa ambayo ni baridi katika misimu yote ya mwaka.

"Njombe inasifika sana kwa baridi, ni vigumu sana kumudu mazingira ya kusoma, wenzangu wengi waliishia njiani. Binafsi niliweka kando uhalisia wa mazingira na niliweza kupata ufaulu mzuri katika matokeo ya mitihani yangu ya kidato cha nne na kupata daraja la kwanza" amesema 'Engineer' Patson.

Ameongeza kuwa mara baada ya kuhitimu masomo yake ya A-Level mwaka 2020, aliweza kufuatilia taarifa za utaratibu wa kujiunga na masomo ya elimu ya juu akiwa kijijini kwao Igolwa, Makete Mkoan Njombe ambapo alijaza fomu ya maombi ya mikopo kupitia mtandao na kuambatisha nyaraka muhimui.

Patson amesema aliamini atapangiwa mkopo wa elimu ya juu kutokana kujaza fomu kikamilifu ambapo mwezi Novemba, 2020 akiwa Chuoni MUST alipata ujumbe kupitia simu ya mkononi kuwa amepangiwa mkopo wa elimu ya juu.

"Mikopo ya elimu ya juu haina upendeleo, jambo kubwa na muhimu ni kujaza fomu kwa usahihi, kutuma kwa wakati na kuweza viambatisho muhimu.

Patson ni miongoni mwa mamia kwa maelfu ya wanafunzi wahitaji wanaonufaika na mikopo ya elimu inayotolewa na Serikali tangu mwaka 1994.

# VYETI 127,292 VYAHIKIKIWA RITA

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA) imesema imehakiki maombi 127,292 ya vyeti vya wanafunzi waombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2022/2023.

Taarifa iliyotolewa Septemba 28, 2022 na Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji wa RITA, Angela Anatory imesema kati ya maombi hayo, maombi 116867 yalikuwa ya vyeti vya kuzaliwa na maombi 18317 yalikuwa ya vyeti vya kifo.

"Kwa mujibu wa utaratibu uliopo, wanafunzi wanaoomba mikopo ya elimu ya juu nchini wanatakiwa kuambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichohakikiwa na Msajili Mkuu wa Vizazi ambapo utaratibu huu pia unawahusisha waombaji kuambatisha cheti/vyeti vya vifo vya wazazi" amesema Angela.

Aidha Angela ameongeza kuwa RITA ilianza rasmi zoezi la uhakiki kupitia mfumo wa uhakiki kwa njia ya kielectroniki tarehe 1 Juni mwaka huu, ambapo jumla ya maombi 135,184 yaliyopokelewa hadi kufikia Septemba 28 mwaka huu.

Kwa mujibu wa Angela amesema katika uhakiki huo, jumla ya maombi 6981 yalibainika kuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo taarifa za vyeti kutoonekana katika kumbukumbu za msajili, kutuma nakala zisizo na namba za ingizo na kuwataka waombaji wenye maombi yenye changamoto kuwasiliana na ofisi za huduma kwa wateja ili kuweza kurekebisha kasoro zilizobainika.

"Wakala umeimarisha huduma katika kitengo kinachoshughulikia maombi ya uhakiki ili kuhakikisha maombi yanajibiwa mara yanapopokelewa hivyo kuwawezesha waombaji kuendelea na taratibu nyingine za kuomba mkopo" amesema Angela.

Ameongeza kuwa RITA inaendelea na mkakati wa kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma zake kwa wateja kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma kwa gharama nafuu.



# HESLB YATETA NA VIONGOZI WA TAHLISO



**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru amewahakikishia viongozi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu (TAHLISO) kuwa HESLB itaendelea kutoa ushirikiano unaohitaji katika kuendelea kuwahudumia wanafunzi vyuoni.

Akizungumza katika kikao kilichofanyika tarehe 31, Agosti 2022 Jijini Dar es Salaam baina yake na viongozi waandamizi wa TAHLISO wakiongozwa na Mwenyekiti wao Frank Nkinda, Badru amesema Serikali kupitia HESLB itahakikisha fedha za mikopo zinaendelea kufika kwa wakati katika vyuo vyote nchini.

"Kama mnavyofahamu, dirisha la maombi ya mikopo kwa mwaka 2022/2023 bado lipo wazi na wanafunzi wanaendelea na mchakato wa maombi. Menejimenti tumejipanga kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenye sifa na vigezo watapangiwa mikopo na fedha zao zitafika kwa wakati" amesema Badru.

Badru amesema katika kipindi cha miaka sita iliyopita, bajeti ya fedha za mikopo ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, ambapo kwa mwaka 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha TZS 573 Bilioni ikiwemo kiasi cha TZS 3 Bilioni zilizotengwa kama ruzuku kwa wanafunzi waliofaulu vizuri masomo ya sayansi kwenye mitihani ya kidato cha sita 2022.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TAHLISO, Frank Nkinda ameishukuru Menejimenti ya HESLB kwa ushirkiano mkubwa inaoendelea kuipatia jumuiya hiyo ikiwemo kushughulikia kwa wakati changamoto zote zinazohusu mikopo kwa wanafunzi.

"TAHLISO inaishukuru HESLB kwa kulipa mikopo ya wanafunzi kwa wakati na pia tumekuwa na ushirikiano mzuri na menejimenti za vyuo hususani maafisa wa madawati ya mikopo katika vyuo wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa kwa Serikali za wanafunzi katika kushughulikia changamoto za wanafunzi" amesema Nkinda.

Katika ziara hiyo, viongozi hao wa TAHLISO pia walipokea taarifa kutoka HESLB kuhusu mchakato wa maombi ya mkopo kwa mwaka 2022/2023. Mbali na mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Viongozi wengine wa TAHLISO walioshiriki ziara hiyo ni pamoja na Makamu wa Rais, Rabia Burhan, Mhazini Mkuu, Chrisma Mwingira na Kamshina wa Mikopo, Emmanuel Martine.



# RAMA

## SAFARI YA KUSIFURISHA TZS 5 MILIONI

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Wahenga walisema Mwenye deni analala mlango wazi, methali hii ilimwamsha na kumnyanyua Mwalimu Ramadhani Uledi (35) na kufika moja kwa moja hadi Ofisi ya HESLB Zanzibar.

Mwalimu Ramadhani Uledi ni mnufaika wa mikopo ya elimu ya juu ambaye alisomeshwa na HESLB katika Chuo Kikuu cha Abdulrahman Sumait kilichopo Chukwani Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar mwaka 2013-2016.

Akizungumza na HESLB Yako, Ramadhani amesema mara baada ya kuhitimu masomo yake ya 2016, miaka miwili baadaye aliajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) na baada ya miezi mitano tangu kuajiriwa alipatiwa taarifa ya deni la mkopo wa HESLB kutoka kwa mwajiri wake.

"Baada ya kupokea taarifa ya deni langu la TZS 11 Milioni nilifika katika Ofisi ya HESLB Zanzibar na kuuliza taratibu za kumaliza mkopo huo moja kwa moja, ambapo kati ya mwaka 2018-2022 nilijikuta nimelipa kiasi cha TZS 6 Milioni" amesema Ramadhani.

Ameongeza kuwa baada ya kupata taarifa ya unafuu uliowekwa na Serikali katika urejeshaji wa mikopo hiyo, mwezi Juni mwaka huu aliamua kufika ofisi za HESLB ili kumaliza kiasi chote cha deni la mkopo huo ili fedha hizo ziweze kuwanufaisha vijana wengine wa Kitanzania.

Mwalimu Ramadhani ambaye ni Mwalimu wa masomo ya Islam na Kiswahili, amesema anaishukuru Ofisi ya HESLB Zanzibar kwa kumpatia ushirikiano mzuri pindi alipofika na kueleza dhamira yake ya kumaliza mkopo huo moja kwa moja kwa kulipa kiasi cha TZS 5 Milioni.

"Wapo waliokuwa na fikra na mtazamo tofauti kuhusu hatua hii ya kulipa deni la HESLB na kumaliza deni hili, nashukuru kwa sasa wenzangu wameanza kunielewa na wengine kuwa na hamasa na mwitikio wa jambo. Mimi nimejitolea kuwa Balozi wa HESLB" amesema Mwalimu Ramadhani.

Mwalimu Ramadhani ameongeza kuwa alitambua majukumu mbalimbali aliyonayo kama Baba na Mume katika kujenga msingi imara wa kipato na uchumi wa familia yake lakini aliguswa na maisha ya vijana wengine waombaji mikopo.

"Nawasihi wanufaika wenzangu tujitokeze turejeshe mikopo yetu kwani kwa kufanya hivi kutasaidia ndugu zetu wanaojiunga katika masomo ya elimu ya juu sambamba na kujenga taifa lenye nguvu katika Nyanja za kijamii na kiuchumi" amesema Mwalimu Ramadhani.

**HESLB**
Loans Board
INVESTING IN THE FUTURE

# Strategic Plan 2022/2023 - 2026/2027

# WE VALUE

## VISION

To become a reliable and sustainable Tanzanian financier for tertiary education students.

## MISSION

To sustainably issue loans and grants to eligible Tanzanians pursuing tertiary education & prudently manage loans collection.

## STRATEGIC THEMES

- Optimal lending and loan collection
- Business re-engineering and automation
- Strategic partnerships

## CORE VALUES

**ACCOUNTABILITY**
We take the initiative to own our responsibilities by pursuing excellence, honouring our commitments and upholding integrity.

**CUSTOMER - CENTRIC**
We are committed to prioritize and timely serve, listen and respond to customers' needs.

**TEAMWORK**
We embrace networking and support one another in pursuit of excellence in serving customers.

**PROFESSIONALISM**
We are qualified, skilled and passionate in delivering our services in accordance with highest standards of ethics.

**INNOVATION**
We constantly develop solutions to address new lessons to meet the evolving needs of our customers.

**EQUITY**
We treat our customers with fairness and respect to promote diversity and inclusion.

HESLB Tanzania | HESLB_Tanzania | 0739 665 533

HEET Higher Education for Economic Transformation | WORLD BANK GROUP

## OUR PROJECT: Higher Education for Economic Transformation

**Description:**

- HEET is a USD. 4 million, five-year (2021/22 – 2025/26) project funded by the World Bank to promote reforms and improved operational capacity and delivery at HESLB.

  The project is steered by the Ministry of Education, Science and Technology
- **Project Development Objective:**
  To strengthen the learning environments and labor market orientation of programs in priority disciplines and the management of the higher education system
- **Component 2:**
  Strengthening the management of the higher education system

**Project Focus Areas**

- Business process re-engineering
- Performance and operational improvements on loans management
- Strengthening coordination and linkages with stakeholders
- Capacity building of staff
- Public-private partnerships
- Developing new policies to support equity, quality and sustainability.

## OUR CONTACT


**DAR ES SALAAM**
HESLB House, 1 Kilimo Street, Tazara Area, Mandela Road,
P.O Box 76068, 15471 Dar es salaam, Tanzania
+255 739 665 533
info@heslb.go.tz

**DODOMA**
PSSSF Building, Makole Road,
Plot No. 4&5, Block W, Uhindini Area,
+255 758 067 577 | +255 739 067 57
dodoma@heslb.go.tz

**ZANZIBAR**
Michenzani Mall Building,
Michenzani Area, Side A,
5th Floor, Hall 501
P.O. Box 900
Zanzibar, Tanzania
+255 779 321414
zanzibar@heslb.go.tz

**MBEYA**
CAG Building, Mbalizi Road
P.O. Box 319
Mbeya, Tanzania
0738 131310
0738 131311
mbeya@heslb.go.tz

**ARUSHA**
NSSF Mafao House, 1st Floor,
P.O Box 2712,
Arusha, Tanzania
+255 27 2520128
+255 624 100011
+255 0739 102016
arusha@heslb.go.tz

**MTWARA**
NHC Raha Leo Complex
2nd floor Plot no. 217 Block H.
Near Regional Commissioner's Office
P.O.Box 969,
Mtwara, Tanzania
Cell: 0736 026 668
mtwara@heslb.go.tz

**MWANZA**
PSSSF Plaza Building, 2nd Floor
Front Wing, Kenyatta Road,
P.O. Box 3051,
Mwanza, Tanzania
+255 28 2506008
+255 759 819350
+255 738 153661
mwanza@heslb.go.tz

**CUSTOMER CENTRE**
PSSSF Twin Towers,
Ground Floor,
Plot 120/121, Mission Street,
P.O. Box 76068,
Dar es salaam.